

SHULE YA SEKONDARI MENGENI

S.L.P 233, MKUU-ROMBO.

Mobile Na: 0766483093

Barua pepe:[mengenisec2007@gmail.com](mailto:mengenisec2007@gmail.com)

Tarehe: .....

KUMB.NA.MSS/JOIN/F.1/VOL.1/

Jina la Mwanafunzi.....

S.L.P.....

.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MENGENI  
WILAYA YA ROMBO MKOA KILIMANJARO MWAKA 2021**

**1.0 Utangulizi**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **kwanza** katika shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Mengeni ipo umbali wa kilometa 15 kutoka mji mkuu wa wilaya ya Rombo.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/1/2020 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/1/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 17/1/2020 ndani ya siku saba.

**2.0 Mambo muhimu kuzingatia.**

Kila mwanafunzi atatakiwa kuwa na Vifaa vifuatavyo:

Madaftari Counter Book (QUIRE THREE) – 10

Madaftari madogo ya kawaida kwa ajili ya mazoezi ya wiki-10

Kalamu za wino na penseli, mkebe wa hesabu, rula na ufuto.

Begi la kubebea daftari lisilo na picha wala maandishi (Mifuko aina ya Rasketi na Bobmarley hairuhusiwi)

Picha 01 ya passport size.

**Masomo atakayofundishwa**

i. Uraia [Civics], ii. Historia [History], iii. Jiografia [Geography], iv. Kiswahili

v. Kiingereza [English], vi. Hisabati [Mathematics], vii. Kemia [Chemistry], viii. Fizikia [Physics]

ix. Elimu ya Viumbe [Biology] x. Kilimo [Agriculture]

**2.1 SARE YA SHULE:**

**A. WAVULANA:**

i. Shati 2 nyeupe za mikono mifupi.

ii. Soksi nyeusi ndefu pea 3 au zaidi zisizo na maua (urembo)

iii.Suruali mbili kitambaa cha rangi ya ugoro (brown).Mshono wa rinda mbili mbele,iwe ndefu na isiwe ya kubana.Pia iweze kukaa kiunoni na isiruhusu kuvaa mlegezo.Upana wa chini kwenye turn-up uwe [INCHI 17]

iv.Viatu pea 2 vyeusi vya kufunga na gidamu vyenye kisigino kifupi

v.Sweta 2 zifanane na rangi ya suruali

vi.Tai 2 za kufunga zilizoshonwa kutoka katika kitambaa cha suruali

#### **B. WASICHANA:**

i.Shati mbili nyeupe za kitambaa cha mikono mifupi.

ii.Soksi nyeupe ndefu zisizoangaza pea 3 au zaidi zisizo na maua (urembo)

iii.Sketi mbili kitambaa cha rangi ya ugoro (brown).Mshono wa rinda box.Urefu wake ufike kwenye kifundo cha mguu.[**Sketi fupi ni marufuku**]

iv.Viatu pea 2 vyeusi vya kufunga na gidamu vyenye kisigino kifupi.

v.Sweta mbili zifanane na rangi ya sketi.

vi.Tai 2 za kufunga zilizoshonwa kutoka katika kitambaa cha sketi.

Rangi ya kitambaa kwa ajili ya sketi imeambatanishwa juu ya fomu ya hii.

#### **C.NGUO ZA MICHEZO:**

i) Track suit (suruali na T-shirt)

ii.Raba za michezo

Sare hizi ni kwa wavulana na wasichana na zitavaliwa wakati wa michezo tu.

#### **2.2 MICHANGO:**

Michango ya chakula na maendeleo ya shule itatokana na makubaliano ya kikao cha wazazi kitakachofanyika shuleni tarehe 05/01/2021 kama Waraka wa Elimu Namba 3 wa Mwaka 2016 unavyoelekeza.

#### **ANGALIZO:**

**1.VIAMBATANISHO 1,2** viletwe shuleni vikiwa vimejazwa kwa usahihi na wahasika

#### **3.0.SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia sheria na kanuni zifuatazo:-

- a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote ,na
- i) Kutunza mali ya umma.

**3.1.MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.**

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevywa kama vile uvutaji wa bangi,cocaine,mirungi,kubeli na kadhalika
- e) Kupigana au kupiga.
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- g) Kudharau Bendera ya Taifa.
- h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
- i) Kuo au kuolewa.
- j) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- k) Kutoa mimba
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- m) Kuwa na simu ya mkononi.

**4.0 MUHIMU:**

- ( i ) Hakikisha mwanafunzi amepimwa afya katika hospitali za Serikali na kujaziwa fomu ya medical examination na hakikisha umepewa risiti za malipo na iambatanishe na fomu husika.
- ( ii ) Endapo mzazi utashindwa kutekeleza masharti yaliyowekwa katika ushonaji wa sare kwa wanafunzi itakugharimu kumshonea mwanao sare nyingine.
- ( iii) Unatakiwa kuhudhuria kikao cha wazazi wa kidato cha kwanza tarehe **05/01/2021 siku ya Jumanne** saa tatu asubuhi bila kukosa.
- (iv ) Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

.....

**MKUU WA SHULE**

**“ FOMU “A”**  
**SHULE YA SEKONDARI MENGENI**  
**FOMU YA MWANAFUNZI / MZAZI YA KUKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA KWANZA**  
**MWAKA.....**

**A.** Mimi.....(Jina la mwanafunzi)

**NINAKUBALI/SIKUBALI** nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari Kilamacho. Ninaahidi kuwa nitatii kanuni na sheria zote za shule na kufuata kikamilifu masharti yote yatakayotolewa na Mkuu wa shule au mwalimu au yeyote mwenye mamlaka shuleni. Ninaahidi pia kwamba nitajitahidi kushirikiana na wenzangu katika shughuli zote za masomo, uzalishaji mali na michezo. Na sitashabikia au kujihusisha na mambo maovu shuleni kama kuanzisha au kuchochea migomo.

**DINI/ DHEHEBU** langu ni .....(Taja kama wewe ni Mkatoliki, Mlutheri, S.D.A, Mwislamu, Pentekoste n.k

.....

**SAHIHI YA MWANAFUNZI**

**B. IJAZWE NA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi) ..... wa (anwani/namba ya simu).....

Nakubali nafasi aliyotunukiwa mwanangu ya kujiunga na SEKONDARI. Ninaahidi vile vile kuwa nitashirikiana na Mkuu wa shule na Walimu kumlea kitabia na kimasomo pia kumtimizia mahitaji yake yote ya shule na nyumbani kwa kadri itakavyohitajika. Pia nitahudhuria vikao vya wazazi shuleni au wito maalumu kwa ajili ya kupata taarifa ya maendeleo na nidhamu ya mwanangu.

.....

**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI**

**TAREHE:.....**

**“FOMU B”**  
**MENGENI SECONDARY SCHOOL**  
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**From: The Headmaster/Headmistress**

**Mengeni Secondary School,**

**P.O.Box 233**

**MKUU-ROMBO**

**Date .....**

The medical officer,  
Government Hospital

Name of the Pupil.....

Please examine the above named Pupil and arrange any necessary treatment so that the certificate can be signed and so that the pupil can return in time for the beginning of the next term or to join form one.

**MEDICAL CERTIFICATE;**

(To be completed by Medical Officer)

I have examine the above named pupil with regard to:-

**REMARKS**

Skin .....

Eyes.....

Ears.....

Teeth.....

Chest .....

Spleen .....

Abdomen .....

Urine .....

Stool .....

HB (Hemoglobin).....

Pregnancy test (for girls).....

Any.Disabilities.....

And consider that:-

1.The pupil is in good health ,free from infections of diseases,worms,bilharzias,and is fit to return to school/to join form one.

2.She/He is now fit to return to school having had treated to join Form One for,

.....

DATE :.....

.....

Name/signature of medical office.